# TUJIFUNZE BIBLIA

## *SOMO LA 11*

### WATUMISHI NA WAANGALIZI WA KANISA

Watu hupenda kupewa heshima na mamlaka kuliko watu wengine. Hata katika siku za Yesu, baadhi ya wanafunzi wake walitaka wapewe cheo kuliko wenzao.

"*Na Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo, wakamwendea, wakamwambia, Mwalimu, twataka utufanyie lo lote tutakalokuomba… Wakamwambia, Utujalie sisi tuketi, mmoja mkono wako wa kuume, na mmoja mkono wako wa kushoto, katika utukufu wako… Yesu akawaita, akawaambia, Mwajua ya kuwa wale wanaohesabiwa kuwa wakuu wa Mataifa huwatawala kwa nguyu, na wakubwa wao huwatumikisha. Lakini haitakuwa hivyo kwenu; bali mtu anayetaka kuwa mkubwa kwenu, atakuwa mtumishi wenu, na mtu anayetaka kuwa wa kwanza wenu, atakuwa mtumwa wa wote.*" Marko 10:35-37,41-44

1. Je! Yesu alikubali kuwapa Yakobo na Yohana cheo au heshima kuliko wenzao? ___________________
2. Mtu ambaye anataka kuwa mkubwa kwetu imempasa kuwa nini? ___________________
3. Mtu ambaye anataka kuwa wa kwanza imempasa kuwa nini? ___________________

"*Saa ile wanafunzi wakamwendea Yesu wakisema, Ni nani basi aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni? Akaita mtoto mmoja, akamweka katikati yao… Basi, ye yote ajinyenyekeshaye mwenyewe kama mtoto huyu, huyo ndiye aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni.*" Mathayo 18:1,2,4

4. Mtu atakayekuwa mkuu katika ufalme wa mbinguni ni yule ajinyenyekeshaye mwenyewe kama nani? ___________________
5. Je! mtu ajinyenyekeshaye atatumia mavazi na majina yanayomtofautisha na Wakristo wengine? ___________________

Yesu aliwaonya wanafunzi wake kuhusu viongozi wanaotaka heshima akisema:

"*Tena matendo yao yote huyatenda ili kutazamwa na watu; kwa kuwa hupanua hirizi zao, huongeza matamvua yao; hupenda viti vya mbele katika karamu, na kuketi mbele katika masinagogi, na kusalimiwa masokoni, na kuitwa na watu, Rabi. Bali ninyi msiitwe Rabi* (yaani, mwalimu), *maana mwalimu wenu ni mmoja, nanyi nyote ni ndugu. Wala msimwite mtu baba duniani; maana Baba yenu ni mmoja, aliye wa mbinguni. Wala msiitwe viongozi; maana kiongozi wenu ni mmoja, naye ndiye Kristo. Naye aliye mkubwa wenu atakuwa mtumishi wenu.*" Mathayo 23:5-11

6. Yesu aliwashitaki viongozi wa Wayahudi kwa sababu walifanya matendo yao yote ili watazamwe na nani? ___________________
7. Viongozi hawa walikuwa wakivaa mavazi tofauti na watu wengine ili wajulikane kuwa watu wa dini. Je! Yesu aliwasifa kwa mavazi yao? (1 Petro 3:3-4) ___________________

8. Je! Neno “rabi” maana yake ni nini? ____________________

9. Mwalimu wa Wakristo ni nani? ____________________

10. Maana ya majina “Papa” na “Padiri” ni “baba”. Je! Yesu alitaka Wakristo waitwe baba katika kanisa lake? ____________________

11. Yesu alisema kwamba Wakristo wawe na viongozi wangapi? ____________________

12. Kiongozi wa Wakristo ni nani? ____________________

13. Mtu aliye mkubwa katika Wakristo atakuwa nani? ____________________

Paulo aliwashitaki Wakristo ambao walikuwa wakiwaheshimu watu wengine kuliko wenzao. Twasoma:

“*Kwa maana, ndugu zangu, nimearifiwa habari zenu wa wale walio wa nyumbani mwa Kloe, ya kwamba iko fitina kwenu. Basi, maana yangu ni hii, ya kwamba kila mtu wa kwenu husema, Mimi ni wa Paulo, na, Mimi ni wa Apolo, na, Mimi ni wa Kefa (yaani, Petro), na, Mimi ni wa Kristo. Je! Kristo amegawanyika? Je! Paulo alisulibiwa kwa ajili yenu? Au Je! mlibatizwa kwa jina la Paulo? ... Basi ndugu, mambo hayo nimeyafanya kuwa mfano wa mimi na Apolo kwa ajili yenu, ili kwamba kwa mfano wetu mpate kujifunza kutokupita yale yaliyoandikwa; ili mmoja wenu asijivune kwa ajili ya huyu, kinyume cha mwenziwe.*”

1 Wakorintho 1:11-13; 4:6-7

14. Je! inafaa kwa Wakristo kumtukuza mtu mmoja kuliko wengine na kujiita kwa jina lake? ____________________

15. Mfano huu wa Petro, Paulo, na Apolo hutufundisha kutokupita nini? ____________________

Ingawa mstari huo umetuonya kutokupita yale yaliyoandikwa katika Biblia, walakini watu fulani wameyapita. Watu hawa huwapa watu cheo na majina kinyume cha maandiko. Kwa mfano, cheo na majina kama Kardinali, archbishop (askofu mkuu), archdeacon (shemasi mkuu), Rais, Papa, Captain (kapiteni), na Reverand ni majina yaliyobuniwa na watu. Biblia haiwaruhusu Wakristo kutumia majina haya bali imetuonya hivyo:

“*Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki.*” Ufunuo 22:18

“*Kila apitaye cheo, wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu.*” 2 Yohana 1:9

16. Je! kuna hatari katika kubuni na kutumia cheo na majina yasiyotajwa katika Biblia? ____________________

Kama tulivyoona huko juu, Mungu hajaweka wakuu katika kanisa bali ameweka watumishi. Katika Biblia watumishi hawa wamejulikana kwa majina yatakayozungumza hapo chini.

“*Naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe.*” Waefeso 4:11-12

17. Taja majina matano ya watumishi tunayoyapata katika mistari hii: ___________________ ___________________ ___________________ ___________________ ___________________

Majina mengine tunayoyasoma katika Biblia ni wazee, waangalizi, mashemasi, makuhani, na watakatifu. Ebu, tuanze kuyachunguza majina haya moja moja.

**MITUME NA MANABII**

Katika somo la 9 tulijifunza jinsi manabii na mitume walivyomaliza kazi yao wakati walipokuwa wakiandika Agano Jipya. Kwa hiyo, hatuna manabii wala mitume katika kanisa leo. Twasoma:

"*Upendo haupungui neno wakati wo wote; bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika.*" 1 Wakorintho 13:8

18. Paulo alisema unabii utafanya nini? ___________________

"*Mmejengwa juu ya msingi wạ mitume na nanabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni.*" Waefeso 2:20

Mtu anapojenga nyumba huanza kwa kuweka msingi. Ikiwa ameweka msingi imara, basi hana haja ya kuweka msingi mwingine. Kanisa limejengwa įuu ya msingi wa mitume na manabii. Msingi ule ule unadumu mpaka leo na, kwa hiyo, hatuna haja ya mitume au mnanabii wapya. La! bali Biblia yatuonya tusidanganywe na mitume na manabii wa uongo.

"(Yesu alisemna) *kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule.*" Mathayo 24:24

"Maana watu kama hao ni mitume wa uongo, watendao kazi kwa hila, wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo. Wala si ajabu. Maana Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru. Basi si neno kubwa watumishi wake nao wakijigeuza wawe mfano wa watumishi wa haki ambao mwisho wao utakuwa sawasawa na kazi zao." 2 Wakorintho 11:13-15

19. Je! mitume wanatakiwa katika kanisa leo? ___________________

20. Je! manabii wa uongo na mitume wa uongo watajaribu kudanganya Wakristo kwa ishara na maajabu? ___________________

**WAINJILISTI, WAHUBIRI, NA WAALIMU**

Majina haya yamefanana sana. Kwa wastani, mwinjilisti ni mtu anayehubiri Injili (habari njema) ya Yesu kwa watu ambao hawajawahi kuisikia. Siku hizi watu wengi humwita mwinjilisti kuwa ni mishonari. Walakini, jina mishonari halimo katika Biblia. Mhubiri na mwalimu ni watu wanaoeleza mafundisho ya Mungu kwa wale waliokwisha kuisikia Injili. Watu hawa wanatakiwa katika kanisa mpaka leo, maana twasoma:

"*Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia kwa kuwa, Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka. Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri? Tena wahubirije, wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa, Ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema!*" Warumi 1:16; 10:13-15

21. Je! wainjilisti, wahubiri, na waalimu wanatakiwa katika kanisa leo? ____________________

**WAZEE, MAASKOFU, WAANGALIZI, NA WACHUNGAJI**

Watanzania hufahamu jinsi Rais Julius K. Nyerere anavyojulikana kwa majina mbalimbali. Kwa mfano anaitwa Mwalimu, Rais, Baba wa TANU, na Baba wa Taifa pia. Majina haya yote yanamhusu mtu yeye yule. Hali kadhalika mzee, askofu, mwangalizi, na mchungaji yote ni majina yanayo mhusu mtu yule anayefanya kazi ya askofu katika kanisa. Ebu! tuhakikishe mambo hayo. Jambo la kwanza, askofu anaitwa pia mzee wa kanisa kwa sababu ni mtu mzima ambaye ameoa, tena anao watoto walio wakubwa kiasi cha kuamini. Twasoma:

"*Kwa sababu hii nalikuacha Krete, ili uyatengeneza yaliyopunguka, na kuweka wazee katika kila mji kama vile nilivyokuamuru; ikiwa mtu hakushitakiwa neno, naye ni mume wa mke mmoja, ana watoto waaminio wasioshitakiwa kuwa ni wafisadi wala wasiotii. Maana imempasa askofu awe mtu asiyeshitakiwa neno, kwa kuwa ni wakili wa Mungu… Basi imempasa askofu awe mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi na mwenye kuisimamia nyumba yake vema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu; (yaani, mtu asiyejua kuisimamia nyumba yake mwenyewe, atalitunzaje Kanisa la Mungu?) Wala asiwe mtu aliyeongoka karibu, asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya Ibilisi.*"

Tito 1:5-7; 1Timotheo 3:2,4-6

22. Je! kijana ambaye hajaoa anaweza kuwa askofu? ____________________

23. Je! Mkristo ye yote aliyezeeka aweza kuitwa mzee wa kanisa? ____________________

24. Je! mtu anaweza kuwa askofu ikiwa watoto wake ni wadogo wasioweza kuamini?

____________________

25. Je! mtu mwenye mtoto mmoja tu aaminiye aweza kuwa askofu? ____________________

26. Je! mtu ambaye amekuwa Mkristo kwa muda mfupi aweza kuwa askofu? ____________________

Jambo, la pili, askofu ni mwangalizi. Unaposoma 1 Timotheo 3:1 katika Biblia yako utaona kwamba chini yake kuna maelezo yanayosema "askofu maana yake ni mwangalizi." Tena, twasoma:

"*Toka Mileto Paulo akatuma watu kwenda Efeso, akawaita wazee wa kanisa. Walipofika kwake, akawaambia, Ninyi wenyewe mnajua tangu siku ya kwanza nilipokanyaga hapa Asia, jinsi nilivyokuwa kwenu wakati wote… Jitunzeni nafsi zenu na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe.*" Matendo 20:17-18,28

27. Paulo aliwakumbusha wazee wa kanisa jinsi Roho Mtakatifu alivyowaweka katika kanisa wawe nini? ____________________

28. Wazee ni waangalizi (maaskofu) wanaotunza na kulisha nini? ____________________

29. Mtu ambaye anatunza na kulisha kundi huitwa mchungaji. Je! mistari tuliyoisoma inaonyesha kwamba mzee wa kanisa ni mchungaji? ____________________

"*Mtume Petro alisema: Nawasihi* <u>*wazee*</u> *walio kwenu,* <u>*mimi niliye mzee, mwenzi wao*</u>*, na shahidi wa mateso ya Kristo, na mshirika wa utukufu utakaofunuliwa baadaye;* <u>*lichungeni kundi*</u> *la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo. Wala si kama wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi. Na* <u>*Mchungaji mkuu*</u> *atakapodhihirishwa, mtaipokea taji ya utukufu, ile isiyokauka.*" 1 Petro 5:1-4

30. Petro aliwasihi wazee wa kanisa walichunge nini? ____________________

31. Mchungaji mkuu wa kanisa ni nani? ____________________

Mistari hiyo inatuonyesha wazi kwamba kila mzee wa kanisa ni askofu, mwangalizi, na mchungaji pia; maana, kazi yake ni kuangalia, na kuchunga, na kutunza, na kulisha kanisa.

Mara yingine, katika Kiingereza, askofu huitwa "Pastor" (Neno "pastor" maana yake ni mchungaji.) Watu fulani wameuasi mpango wa Mungu wakimwita mhubiri wao kuwa pasta. Lakini si halali kumwita mtu pasta isipokuwa ameyatimiliza kwanza masharti yote ya askofu wa kanisa yaliyoandikwa katika 1Timotheo 3:1-7 na Tito 1:5-8. Vivyo hivyo, mtu hawezi kuitwa mzee wa kanisa isipokuwa ameyatimiliza masharti hayo yote.

32. Je! ni halali kumwita mtu pasta ikiwa hajahitimu masharti au sifa za askofu?

____________________

33. Je! Mkristo ye yote aliyezeeka anaweza kuitwa mzee wa kanisa? ____________________

34. Je! askofu, mwangalizi, mzee wa kanisa, na mchungaji (yaani, pasta) yote ni mamoja?

____________________

Wako watu wanaotaka kubadili mpango wa Mungu wakijaribu kutofautisha kati ya majina haya. Tena, huwakataza maaskofu na watu wengine wasioe wakisema Mungu amewaruhusu kubadili mambo haya. Tuone ikiwa Mungu amewaruhusu:

"*Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho* <u>*wengine watajitenga na imani*</u>*, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani; kwa unafiki wa watu wasemao uongo wakichomwa moto dhamiri zao wenyewe;* <u>*wakiwazuia watu wasioe*</u>*, na kuwaamuru wajiepushe na vyakula, ambavyo Mungu aliviumba vipokewe kwa shukrani na walio na imani wenye kuijua hiyo kweli.*" 1 Timotheo 4:1-3

35. Watu wale wanaowazuia wenzao wasioe ni watu wanaosikiliza mafundisho ya nani?

____________________

## MASHEMASI

Shemasi maana yake ni mtumishi wa kanisa. Matendo 6:1-6 ni mfano wa kazi yao. Mtu hawezi kuitwa shemasi isipokuwa ameyatimiza kwanza mambo yale yaliyoandikwa hapo chini. Twasoma:

"*Vivyo hivyo mashemasi na wawe wastahivu; si wenye kauli mbili, si watu wa kutumia mvinyo sana, si watu wanaotamani fedha ya aibu; wakiishika siri ya imani katika dhamiri safi. Hawa pia na wajaribiwe kwanza; baadaye waitende kazi ya shemasi, wakiisha kuonekana kuwa hawana hatia. Vivyo hivyo wake zao na wawe wastahivu; si wasingiziaji; watu wa kiasi; waaminifu katika mambo yote. Mashemasi na wawe waume wa mke mmoja, wakiwasimamia watoto wao vizuri, na nyumba zao.*" 1 Timotheo 3:8-12

36. Je! mtu ambaye hana watoto anaweza kuwa shemasi? ____________________

37. Je! mtu anaweza kuwa shemasi ikiwa mke wake si Mkristo? ____________________

## KUHANI MKUU NA MAKUHANI

Mtu mmnoja tu anaweza kuwa kuhani mkuu. Kazi ya kuhani mkuu ni kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi. Twasoma:

"*Basi, iwapo <u>tunaye kuhani mkuu</u> aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu… Maana kila kuhani mkuu huwekwa ili atoe vipawa na dhabihu; kwa hiyo lazima huyu naye awe na kitu cha kutoa… Lakini Kristo akiisha kuja, aliye kuhani mkuu wa mambo mema yatakayokuwapo, kwa hema iliyo kubwa na kamilifu zaidi, isiyofanyika kwa mikono, maana yake, isiyo ya ulimwengu huu, wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe, aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele… Kwa sababu Kristo hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa patakatifu halisi, bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu; <u>wala si kwamba ajitoe mara nyingi</u>, kama vile kuhani mkuu aingiavyo katika patakatifu kila mwaka kwa damu isiyo yake; <u>kama ni hivyo, ingalimpasa kuteswa mara nyingi tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu</u>; lakini sasa, <u>mara moja tu</u>, katika utimilifu wa nyakati, amefunuliwa, azitangue dhambi kwa dhabihu ya nafsi yake.*" Waebrania 4:14; 8:3; 9:11-12,24-26

38. Kuhani mkuu wetu ni nani? ____________________

39. Yesu alitoa dhabihu gani kwa ajili yetu? ____________________

40. Je! dhabihu hii imetosha au inatakiwa tuzidi kutoa nyingine? ____________________

41. Je! tunapokula chakula cha Bwana tunamtoa Yesu tena awe dhabihu? (1 Wakorintho 11:23-26) ____________________

Baadhi ya watu husema kwamba katika kanisa watu wachache tu ni makuhani wanaoweza kubatiza watu, kutoa chakula cha Bwana, na kadhalika. Walakini, Biblia hufundisha kwamba <u>kila Mkristo ni kuhani</u>.

"*Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake, na kutufanya kuwa ufalme, na <u>makuhani</u> kwa Mungu, naye ni Baba yake; utukufu na ukuu una Yeye hata milele. Amin.*" Ufunuo 1:5-6

"*Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejeng wa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazokubaliwa na Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo… Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu.*" 1 Petro 2:5,9

42. Je! Wakristo wote ni raia wa ufalme wa Yesu? ___________________

43. Je! Wakristo wote ni makuhani? ___________________

## WATAKATIFU

Maana ya neno TAKATIFU ni kitu kilichotengwa. Mtu anapokuwa Mkristo hutakaswa au kutengwa na dhambi. Kwa hiyo, kila Mkristo aliye mwaminifu anaweza kuitwa mtakatifu. Twasoma:

"*Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao.*" Waebrania 12:14

44. Mtu asiyekuwa mtakatifu atamwona Mungu? ___________________

"*Kwa hiyo, ndugu watakatifu, wenye kuushiriki mwito wa mbinguni, mtafakarini sana Mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, Yesu.*" Waebrania 3:1

45. Je! mtu anaweza kuitwa Mtakatifu kabla hajafa? ___________________

## WANAWAKE KATIKA KANISA

"*Mwanamke na ajifunze katika utulivu, akitii kwa kila namna. Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala mwanamume, bali awe katika utulivu.*" 1 Timotheo 2:11-12

"*Wanawake na wanyamaze katika kanisa maana hawana ruhusa kunena, bali watii, kama vile inenavyo torati nayo. Nao wakitaka kujifunza neno lo lote, na wawaulize waume zao wenyewe nyumbani mwao; maana ni aibu wanawake kunena katika kanisa.*" 1 Wakorintho 14:34-35

46. Je! mwanamke anaruhusiwa kuhubiri au kuliongoza kanisa? ___________________

Mistari hii inaonyesha waziwazi ya kwamba mwanamke hawezi kusimama mbele ya kanisa kuhubiri wala hawezi kutawala juu ya wana ume. Hata hivyo, anaweza kufundisha watoto na wanawake wenzake. Tena. anaweza kumsaidia mume wake kufundisha watu nyumbani mwao. Twasoma:

"*Vivyo hivyo na wazee wa kike wawe na mwenendo wa utakatifu; wasiwe wasingiziaji, wasiwe wenye kutumia mvinyo nyingi, bali wafundishao mema; ili wawatie wanawake vijana akili, wawapende waume zao, na kuwapenda watoto wao.*" Tito 2:3-5

Kama tulivyojifunza huko juu, mwanamke hawezi kuwa askofu (mzee wa kanisa) bali wanawake hawa wanaitwa "wazee" kwa sababu ya miaka ya umri wao.

47. Je! wanawake wanaweza kuwafundisha watoto na wanawake wenzao neno la Mungu? ____________________

“(Apolo) *Akaanza kunena kwa ujasiri katika sinagogi; hata* <u>*Prisila*</u> *na Akila walipomsikia* <u>*wakamchukua kwao*</u>, *wakamweleza njia ya Bwana kwa usahihi zaidi.*” Matendo 18:26

48. Je! mwanamke anaweza kumsaidia mume wake kumfundisha mtu neno la Mungu nyumbani mwake? ____________________

*************************************************************************************

Jina lako …………………………………………………

Anwani yako ……………………………………………

***KANISA la KRISTO***
***Tanzania***